BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 30 Mei, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2023/2024.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa Mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

61. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Kwa muda mrefu sasa kumekithiri vitendo vya kufunga wanyama na vitendo vyengine viovu katika maeneo mbali mbali ya makaburi hususan makaburi ya Mwanakwerekwe.

    Je, Wizara yako imejipanga vipi katika kulikomesha jambo hili.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

137. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Itakumbukwa kuwa mnamo mwezi wa Disemba, 2020, Serikali iliwasimamisha kazi watendaji wote wa Kitengo cha Uratibu wa Mradi wa ZUSP (PMT) kufuatia maamuzi ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa kuwa siku nyingi zimepita bila ya watendaji hao kuelezwa kosa lao, na kwa kuwa watendaji hao tangu walivyosimamishwa kazi hawalipwi fedha yoyote na Serikali, na kwa kuwa watendaji hao walikuwa wanategemea fedha za mshahara kuendeshea maisha yao ya kila siku na kwa kuwa watendaji hao wamezungukwa na watu wengi ambao wanawategemea.

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatoa kauli gani kuhusiana na suala hilo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

109. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Iliwahi kuelezwa kuwa, ujenzi wa barabara ya Kiungoni Tovuni kwa kiwango cha lami ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii ya Pwani ya Zanzibar, na mradi wa Tuta la kuzuia maji chumvi la Tovuni katika shehia ya Kiungoni ndani ya jimbo la Pandani. Hata hivyo, hadi sasa hakujaonekana maendeleo yanayoridhisha ya ujenzi huo na badala yake, kupitia Mradi wa TASAF, wananchi wamekuwa wakiitengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha mchanga.

(a) Je, Mradi wa Ujenzi wa barabara ya Kiungoni-Tovuni kwa kiwango cha lami kupitia Mradi wa Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii ya Pwani ya Zanzibar, umefikia wapi.

(b) Je, kwa kiasi gani kumekuwa na ushirikishwaji wa watu wa shehia ya Kiungoni kwenye kazi za vibarua katika mradi huu.

(c) Je, kuna uhusiano gani kati ya Mradi wa TASAF wa kutengeneza barabara hii ya Kiungoni-Tovuni kwa kiwango cha mchanga na ule Mradi wa kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami kupitia Mradi wa Uhimilivu wa

Mabadiliko ya Tabianchi kwa jamii ya pwani ya Zanzibar.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

246. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa kuwa zao la nazi limekuwa tatizo kubwa katika visiwa vya Unguja na Pemba kiasi ambacho bei yake inapanda siku hadi siku na hivyo wananchi wengi kushindwa kulitumia zao hilo pamoja na wengi wao kuwa na uhitaji mkubwa wa kulitumia. Na kwa kuwa minazi mirefu yenye asili ya mwambao wa Afrika Mashariki (East Africa Tall) ina muda mrefu wa kuishi, uwezo mkubwa wa kuzaa pamoja na kuhimili mabadiliko ya tabia nchi. Na kwa kuwa hivi sasa zaidi ya asilimia 70 ya minazi hiyo imeshaanza kupotea na hivyo kubakia minazi chotara (High Breed) inayoshindwa kuhimili mabadiliko ya tabianchi pamoja na kutoa mazao machache mno.

(a) Je, Serikali inalitambua jambo hilo kwa kiwango kipi.

(b) Je, ni juhudi gani zilizochukuliwa na Serikali kuirejesha minazi asilia ya “East African Tall”.

**<u>Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:</u>**

177. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Je, kuna tafiti zozote zilizofanyika kujua sababu za uwepo wa watoto wa mitaani Zanzibar.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

4. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Wanafunzi wa shehia ya Shakani na Buyu hufuata huduma ya elimu kwa masafa marefu, hali inayopelekea kuwepo kwa changamoto tofauti ikiwemo masuala ya udhalilishaji na ufaulu mdogo.

Je, ni lini Serikali itajenga skuli ya msingi kwa ajili ya kuondosha changamoto za aina hiyo kwa wanafunzi na wazazi wa maeneo hayo.

80. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika skuli ya Mtangani Msingi, kuna banda moja la skuli ambalo ni bovu kwa muda mrefu sasa na Wizara yako imetowa amri kuwa watoto hao waingizwe kwenye banda hilo kwa ajili ya kusomea huku ikijuulikana wazi kuwa, nafasi tuliyonayo hivi saa ni ndogo sana.

(a) Je, Wizara yako inalifahamu vipi suala hili.

(b) Ni lini banda hilo litajengwa.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

203. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kuwa suala la mchanga Zanzibar limekuwa na changamoto ya kutopatikana kiurahisi.

(a) Je, ni ipi takwimu ya upatikanaji na mahitaji ya mchanga kwa kipindi cha 2020-2023.

(b) Je, kwa nini Serikali haitengenezi utaratibu wa kuwezesha uchukuaji wa mchanga kutoka ardhi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyoko Makurunge/Bagamoyo.

(c) Je, ni ipi takwimu ya mapato kutokana na mchanga kwa kipindi cha 2020-2023 kwa mamlaka tafauti za Serikali zinazopata mgao.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2023/2024.

Zanzibar,
30 Mei, 2023.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA